# JARIDA LA ZURA

Toleo Nam. 003
Juni 2023

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)



## ZURA ni msimamizi na mtetezi wa wawekezaji wenye ufanisi

UK. 17

**ZURA yashajihisha matumizi sahihi na salama ya Gesi ya kupikia (LPG) Zanzibar**

UK.12

**Udhibiti katika sekta ya umeme utachochea maendeleo ya Nchi kwa kuvutia uwekezaji**

UK. 7

Haliuzwi

ZURA
Zanzibar Utilities Regulatory Authority

www.zura.go.tz




# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| UK. 3. | Udhibiti sekta ya maji utasaidia kupunguza kiwango kikubwa cha upotevu wa maji (non-revenue water) |
| UK. 7. | Udhibiti katika sekta ya umeme utachochea maendeleo ya nchi kwa kuvutia uwekezaji |
| UK. 12. | Zura yashajihisha matumizi sahihi na salama ya gesi ya kupikia (lpg) zanzibar |
| UK. 17. | Zura ni msimamizi na mtetezi wawekezaji wenye ufanisi |
| UK. 23. | Zura yatandika uwanja wa ushindani wa kukuza uchumi |
| UK. 28. | Zura yatumia mfumo wa udhibiti |




## Bodi ya Wahariri




**Mhariri Mkuu:**
Yussuf Khamis Yussuf

**Msaidizi Mhariri Mkuu**
Hussein Seif Dadi

**Waandishi:**
Mbarak Hassan Haji
Shara Chande Omar
Ahlam Saleh Khamis

**Mpiga Picha**
Rahma Hassan Thabit
Mwajuma Alphan Shaame

**Msanifu**
Othman Mohammed Kisawaga

**Msambazaji**
Salum Shomari Salum
Othman Ali Suleiman



*ZURA Headquaters,*
*Nyerere Road, Maisara, Zanzibar - Tanzania*
*S.L.P: 2238*
*+255 24 294 1190*
*info@zura.go.tz*
*ZURA*
*zura_mamlaka*
*zura_mamlaka*
*www.zura.go.tz*



Bw. Omar Ali Yussuf

# UJUMBE WA MKURUGENZI MKUU

Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), inawashukuru sana wananchi wa Zanzibar kwa ushirikiano wa hali ya juu wanaoutoa kwa Mamlaka tangu kuanzishwa kwake. Mamlaka imepata ushirikiano kutoka kwa wananchi wote wa Zanzibar na kuifanya taasisi hii itekeleze majukumu yake vizuri na kwa ufanisi zaidi.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati, Zanzibar (ZURA) ni Mamlaka huru ya udhibiti iliyoanzishwa chini ya kifungu namba 3(1) ya Sheria nambari 7 ya Mwaka 2013. Jukumu la msingi la Mamlaka ni kudhibiti kiuchumi na kiufundi sekta za Maji na Nishati (Umeme, Mafuta na Gesi) ndani ya Zanzibar.

Kwa ajili ya kutimiza malengo yake kwa ufanisi, ZURA inaendelea kutoa Jarida lake maalum ambalo ni Tolea Nam:003 kwa lengo la kuwafikia kirahisi walengwa wake wakubwa ambao ni Wananchi. Madhumuni ya kuanzisha Jarida hili kuwapatia wananchi taaluma na ufahamu juu ya majukumu ya ZURA.

Aidha, majukumu mengine ya Mamlaka ni kupanga bei za huduma za Maji, Umeme na Gesi na pia kuhakikisha wananchi wanazimudu kulingana na huduma zinazotolewa.

Tangu kuanzishwa kwake, ZURA imekuwa na mafanikio mengi, miongoni mwa mafanikio hayo ni upatikanaji wa uhakika kwa bidhaa zote za petroli Zanzibar, uandaaji wa Kanuni za Udhibiti katika sekta zinazodhibitiwa, uanzishaji wa Mfumo Jumuishi wa Udhibiti wa ZURA (ZIRS), ukaguzi wa mara kwa mara wa miundombinu kwa lengo la kudumisha na kuboresha huduma hizo, ufanyaji wa mikutano ya wadau ili kusikiliza maoni na kupokea na kuskiliza malalamiko ya watumiaji.

ZURA ina nia na utayari wa kukupa njia ya urahisi wa huduma zenye kiwango cha hali ya juu na kuwapa umuhimu wananchi kwa kuwapatia mahitaji yao kama wanavyotarajia.

Ni mategemeo yetu kwamba Jarida hili Maalum la ZURA Toleo Nam. 003 litachochea na kuongeza uelewa wa kazi na shughuli za Mamlaka. Kwa mnasaba huu, nitahakikisha kuwa wafanyakazi wa ZURA watasimamia maadili yetu ambayo ni muhimu katika kutimiza ahadi zetu kwa viwango vya utoaji wa huduma vilivyowekwa katika Kanuni na Sheria zetu.

Napenda pia kuwaomba wateja wetu na wadau wengine watupatie maoni juu ya utendaji wetu, maoni hayo yanaweza kuwa ya pongezi, malalamiko, maoni au taarifa juu ya uzoefu wako unaposhirikiana nasi katika huduma zetu zote tunazozidhibiti. Kwa kufanya hivyo itaiwezesha ZURA kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa lengo la kufikia Dira yetu.



# Udhibiti sekta ya maji utasaidia kupunguza kiwango kikubwa cha upotevu wa maji (Non-revenue water)

Watendaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) wakifukia mabomba ya maji safi ili kufanikisha upakinaji wa maji vijijini

**Na: Shara Chande Omar**

Moja ya majukumu ya Mamlaka ni Wizi wa maji, uunganishaji usio halali usiofuata taratibu na vibali, ni mambo ambayo hupelekea mapungufu ya ukusanyaji wa mapato kutokana na huduma hii na hivyo kuwa makusanyo madogo yasiyoakisi gharama halisi zilizotumika kuzalisha na kusambaza maji hayo.

Changamoto zinazopelekea kuongezeka kwa kiwango kikubwa cha upotevu wa maji ni pamoja na hizi zifuatazo: - Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) ni kuhakikisha inasimamia huduma zinazotolewa na sekta na Taasisi inazozidhibiti kwa lengo la kulinda maslahi na manufaa ya watumiaji, sambamba na kuhakikisha huduma hizo zinatolewa kwa ufanisi wenye kuzingatia viwango vya ubora wa huduma husika.

Ingawa kuna jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na watoa huduma katika kuhakikisha wanatoa huduma bora na zenye viwango, bado baadhi ya huduma muhimu kama vile ya maji inayotolewa na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) inakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo ya upotevu wa kiwango kikubwa cha maji (Non-revenue water).

Inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 50% ya maji inapotea hali ambayo huathiri ufanisi na ubora wa upatikanaji wa huduma hiyo muhimu kwa wananchi.

Hali hii ya upotevu mkubwa wa kiwango cha

Inaendelea Uk. 4



maji sio tu inaathiri upatikanaji wa huduma hii muhimu kwa wananchi, lakini pia huisababishia hasara kubwa Mamlaka ya Maji.

Hasara hii hupatikana kuanzia katika gharama inayotumika katika utabibu wa maji haya kuyafanya yawe safi na salama kwa matumizi ya binaadamu ambapo mara nyingi maji haya hupotea wakati wa usambazaji kwa wananchi hatua ambayo yanakuwa tayari yameshatibiwa.

Kadhalika, maji haya hutumia gharama kubwa za umeme kuanzia uzalishaji wake na usambazaji wake hadi kuwafikia wananchi, ambao ni walengwa wakuu wa huduma hii muhimu.

Ingawa kuna jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na ZAWA katika kupunguza tatizo hili ikiwemo ubadilishaji wa mabomba ya maji yaliyochakaa na uwekaji wa miundombinu mipya ya maji, bado inakabiliwa na changamoto nyengine zinazopelekea kuongezeka kwa upotevu huu wa maji.

1)Uchakavu wa miundombinu na mabomba ya kusambazia maji, hali ambayo hupelekea upasukaji na uvujaji wa maji wa mara kwa mara.

2) Uunganishaji holela (wizi) wa huduma ya maji pasi na kufuata taratibu za uungaji wa huduma ya maji zilizowekwa na ZAWA.

3) Kukosekana kwa dira (mita) za maji kwa wateja wanaopatiwa huduma hii na hivyo kuathiri utambuzi na mustakbali mzima wa kiwango cha matumizi ya mtumiaji hali ambayo hupelekea kupewa bili ya makisio au “flate rate” (Commercial loss)

4) Kuwepo kwa wateja sugu wasiochangia au kulipia

5) Kukosekana kwa takwimu halisi ya watumiaji wanaopata huduma hii

Inaendelea Uk. 5



ZURA

Mradi wa usamabazaji Maji safi na salama



Watendaji wa Mamlaka ya maji Zanzibar wakibadilisha mashine katika kisima cha maji kilichopo

kunakosababishwa na uunganishaji wa maji usiofuata taratibu za uungaji wa maji uliowekwa na Mamlaka husika.

6) Uchakavu wa mita zilizofungwa kwa kipindi kirefu hali ambayo hupelekea kukosekana kwa taarifa halisi ya matumizi (Apparent loss).

Katika kukabiliana na hali hii Mamlaka ya Maji Zanzibar ikiwa ni muhusika mkuu, tayari imeanza jitihada za upunguzaji wa kiwango cha upotevu wa maji kwa kulaza mabomba mapya ya maji katika maeneo tofauti. Hatua zinazochukuliwa ni pamoja na utoaji wa elimu juu ya kufuata taratibu za uunganishaji wa maji na kuepukana na wizi ama uunganishaji wa maji unaofanywa kiholela.

Aidha, Mamlaka imeandaa Kanuni na miongozo itakayosaidia kuweka viwango vya ubora wa huduma na maelekezo juu ya namna utoaji wa huduma bora na utekelezaji wa masuala ya kiufundi na upunguzaji wa kiwango cha maji yanayopotea.

Muongozo wa ushindani kwa watoa huduma (Performance benchmarking) ambao utakuwa chachu ya kuongeza uwajibikaji na ufanisi kwa kila mtoa huduma umeandaliwa.

Muongozo huo ambao unakwenda sambamba na miongozo ya kiuchumi yenye lengo la kuweka uwiano wa kibiashara na ushindani wa watoaji huduma kwa kuzingatia gharama na faida katika utoaji huduma bila kumuathiri mtumiaji, utasaidia pia kuongeza jitihada na muamko kwa Mamlaka ya Maji Zanzibar katika kupunguza kiwango kikubwa cha upotevu wa maji.

Kufanya ukaguzi katika vyanzo na miundombinu ya maji kwa lengo la kubaini ufanisi na ubora wa huduma inayotolewa na watoa huduma ya maji, sambamba na kubainisha athari zitakazopelekea uharibifu wa miundombinu na usalama wa huduma ya maji. Vile vile, miongozo hiyo itasaidia pia kuweka utaratibu wa kutoa taarifa za awali juu ya hatua za kukabiliana na upotevu wa maji.

Mwisho.




Umelipa
Bili ya Maji?
*150*01#
"Anza WIKIENDI ukiwa huna Deni na Sisi"
LIPA BILI YAKO KUPITIA
tigo pesa
PBZ BANK
CRDB BANK
NMB
NBC
National Bank of Commerce

# Udhibiti katika sekta ya umeme utachochea maendeleo ya nchi kwa kuvutia uwekezaji



Waziri wa Maji Nishati na Madini Mhe. Shaibu H. Kaduara (Kulia) na Mkurugenzi Mkuu wa ZURA Mhe. Omar Ali. Yussuf (kushoto) Katika shughuli ya kuwapelekea Umeme Wanakijiji wa Kutukuu, Wambaa Pemba

ZURA

**Na: Mbarak Hassan Haji**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) miongoni mwa majukumu yake ni kuhakikisha mtoa huduma za umeme anatoa huduma kwa kuzingatia ubora na uhakika wa uwepo wa huduma husika, vilevile mteja anatumia huduma za umeme bila ya kuathiri ubora husika na kwa kuzingatia taratibu na sheria zilizopo. ZURA kupitia Divisheni ya Umeme inafuatilia kwa karibu watoa huduma za umeme na kuwa karibu na wananchi ili kuhakikisha huduma zinazotolewa ni bora, endelevu na zinapatikana kwa uhakika.

ZURA katika kuhakikisha inafikia malengo yake katika sekta ya umeme hutekeleza majukumu yake ya kazi kama ifuatavyo: -

**Kufanya ukaguzi wa miundombinu ya umeme**

Ili kuhakikisha huduma zinazotolewa kwa wananchi wa visiwa vya Zanzibar ni bora na endelevu ZURA inafanya ukaguzi wa miundombinu ya umeme Unguja na Pemba kwa lengo la kuhakikisha huduma za umeme zinawafikia wananchi kwa ubora na usalama. Miongoni mwa miundombinu inayokaguliwa ni mfumo wa kusafirisha umeme, mfumo na vituo vya kusambazia umeme, pamoja na mifumo ya kuwaunganisha wateja. Hii inasaidia kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wateja na wananchi kwa jumla

Inaendelea Uk. 8

katika maeneo mbali mbali ya visiwa vya Unguja na Pemba.

**Kutowa leseni na vibali kwa watoa huduma za umeme**
Katika kuhakikisha huduma zinazotolewa ni bora, zenye uhakika na endelevu, Mamlaka hutoa vibali na leseni kwa watoa huduma au wadau wanaotaka kuwekeza katika sekta ya uzalishaji nishati ya umeme, usafirishaji nishati ya umeme, usambazaji na uuzaji wa nishati ya umeme. Hatua ya kuwapatia leseni watoa huduma za umeme inaongeza ufanisi wa udhibiti wa huduma zinazodhibitiwa, inahamasisha uwekezaji na kuwalinda wawekezaji katika sekta ya umeme pamoja na kulinda haki za watumiaji wa huduma husika. Hii inamaanisha kuwa mtu yeyote ambaye atafanya uzalishaji, usafirishaji, usambazaji au uuzaji wa huduma ya umeme bila ya leseni au kibali kutoka ZURA, atakuwa amefanya kosa kisheria. Mtu yeyote anayezalisha umeme kwa ajili ya biashara analazimika kuomba leseni kutoka ZURA.

Anayezalisha umeme kwa matumizi binafsi hadi kufikia kilowati 250, atalazimika kuomba kibali ZURA na chini ya hapo atafanya usajili kwa kutaja kiwango anachozalisha. Hata hivyo, kama mtu atazalisha baina ya Kilowati 1 mpaka Kilowati 10 atapata Kibali badala ya Leseni baada ya kufafanya usajili. Kwa wasafirishaji, wasambazaji na wauzaji wakubwa wa umeme watalazimika kuomba leseni kutoka Mamlaka.

**Kupanga bei za umeme**
Mamlaka kupitia Bodi ya Wakurugenzi imepewa Mamlaka kisheria kupanga bei za huduma zote ikiwemo umeme, ambapo mtoa huduma atawasilisha makadirio ya bei kwa Mamlaka. ZURA itapitia bei husika na kuitisha kikao cha wadau kwa ajili ya kujadili bei hiyo na baadae kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya Nishati kwa ajili ya kuanza kutumika.

**Kupitisha mikataba ya mauziano ya nishati ya umeme**
Ili kuhakikisha kuwa mwananchi atapata huduma ya umeme kwa bei nafuu, ZURA imepewa Mamlaka ya kuridhia na kuipitisha mikataba inayofungwa baina ya taasisi zinazouziana nishati ya umeme.

**Changamoto zilizopo katika sekta ya umeme**
Imebainika kwamba matumizi ya umeme katika visiwa vya Zanzibar yanazidi kuwa makubwa siku hadi siku. Hali hii inasababishwa na kuongezeka kwa mahitaji ya umeme kutokana na ongezeko kubwa la miradi mipya inayojengwa kila siku. Miongoni mwa miradi hiyo ni ujenzi wa majengo makubwa kwa ajili ya ofisi za serikali au makazi ya wananchi, ujenzi wa hoteli, ujenzi wa majengo ya kibiashara (Malls), ujenzi wa viwanda vidogo vidogo na vya kati, kuongezeka kwa miji mipya, ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege pamoja na ujenzi unaotarajiwa kuanza karibuni wa bandari ya Mangapwani.

Kukua kwa mahitaji haya kunapelekea kuzidiwa kwa uwezo wa vyanzo vinavyotumika kuleta umeme Zanzibar na hivyo kupelekea kuibuka kwa changamoto mbalimbali katika sekta ya umeme. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama ifuatavyo:
Umeme mdongo: Maeneo mengi ya Zanzibar yanalalamikiwa kuwa na umeme mdogo kiasi cha wananchi kushindwa kupata huduma hiyo kwa uhakika na kupelekea kushindwa kufanya shughuli zao za kiuchumi ambazo huwasaidia kuingiza kipato kwa ajili ya kujikimu kimaisha. Hali hii inasababishwa na kuharibika kwa "Transfoma" mara kwa mara, mwananchi kuunganishwa na mtandao kwa umbali mkubwa kutoka kwenye "Transfoma" husika au mgawanyo wa wateja katika "transfoma" kutokuwa na uwiyano.

Kuchakaa kwa miundombinu ya kusambazia umeme: Kuchakaa kwa miundombinu ya kusambazia umeme imekuwa ni miongoni mwa changamoto kubwa kiasi cha kupelekea huduma ya umeme kwa baadhi ya maeneo kutokuwa ya uhakika, miongoni mwa athari za uchakavu wa miundombinu ni

Inaendelea Uk. 9

kuanguka kwa nguzo mbovu, kuungua kwa baadhi ya vifaa katika mfumo wa kusambazia umeme n.k. hali hii hupelekea kukatika kwa umeme mara kwa mara na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi na baadhi ya wakati hupelekea kuungua kwa baadhi ya vifaa.

**Kuzimwa kwa umeme mara kwa mara:** Kuzimwa kwa umeme mara kwa mara imekuwa ni changamoto kubwa kwa baadhi ya maeneo na kupelekea malalamiko mengi miongoni mwa wananchi. Hali hii inatokana na sababu tofauti ikiwemo zilizopo kwenye utaratibu wa Shirika la Umeme kwa maana ya kufanya matengenezo au sababu ambazo hazipo katika mipangilio ya Shirika la umeme ikiwemo ajali za kuanguka kwa miti inayopelekea kuathiri miundombinu ya umeme au kuungua kwa miundombinu hiyo kutokana na sababu hizo. Hali hii si nzuri hasa kwa uchumi wa nchi kwani kazi nyingi husimama na kuwakosesha huduma wananchi wa kawaida wanaotegemea umeme ili kufanya shughuli zao za kiuchumi kwa ajili ya kujiingizia kipato.

**Kuwepo kwa vituo vichache vya kutoa huduma za umeme:** Pamoja na Shirika la Umeme Zanzibar kuongeza wigo wa kununua umeme kwa njia ya mtandao wa simu na kuanzisha mitandao ya kijamii ili kuwaongezea wigo wananchi wa kutoa na kupokea taarifa, bado kumekuwa na mamalamiko juu ya uwepo wa ofisi chache za kutolea huduma. Mamlaka imelichukua suala hilo na kuliwasilisha kwa wahusika wa Shirika la Umeme na kuahidi kuwa suala hilo linafanyiwa kazi ili kuziwezesha Ofisi za Wilaya kuweza kujitosheleza katika kutoa huduma ili kuwapunguzia usumbufu wananchi wa kufuata huduma makao makuu ya Shirika la Umeme ikiwemo maombi mapya ya kuunganishiwa umeme na kuwasilisha malalamiko hasa wakati wa dharura.

Inaendelea Uk. 10



Wakaguzi wa Umeme kutoka ZURA wakishirikiana na mfanyakazi wa ZECO katika ukaguzi wa Miundombinu ya Umeme



Bodi ya Wakurugenzi wa ZURA wakifanya Ziara katika kituo cha kupozea Umeme Mtoni Unguja

**Hatua zinazochukuliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar**

Mamlaka katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora, salama na endelevu imekuwa ikidhibiti kwa karibu sana watoa huduma za Nishati ikiwemo nishati ya umeme kwa kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo. Mamlaka imekuwa ikifanya ufuatiliaji wa karibu kuhusu huduma zinazotolewa na Shirika la Umeme Zanzibar ili kuhakikisha malalamiko ya umeme kutoka kwa wananchi yanapungua kwa kiwango kikubwa na yale yanayojitokeza basi yanafanyiwa kazi kwa ufanisi ili kuhakikisha huduma zinazotolewa ni bora na zinachangia katika kukuza uchumi wa visiwa vya Zanzibar. Mamlaka imekuwa ikifanya ukaguzi wa miundombinu ya umeme mara kwa mara katika maeneo mbalimbali ya visiwa vya Unguja na Pemba hasa kwenye maeneo ambayo yanachangamoto mbalimbali za umeme na kuhakikisha changamoto hizo zinafanyiwa kazi. Miongoni mwa juhudi zilizofanywa na Mamlaka ni kuyatambua maeneo yote yenye changamoto za umeme mdogo, kuyakagua pamoja na kuyatafutia suluhisho kutoka Shirika la umeme. Aidha, Mamlaka imekuwa ikipokea malalamiko kutoka kwa wananchi wa maeneo mbali mbali na kuambatana nao katika ukaguzi wa maeneo husika na kuyatafutia ufumbuzi malalamiko husika. Miongoni mwa maeneo yaliyokaguliwa ni Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja, Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja, Wilaya ya Kaskazini 'B' Unguja, Wilaya ya Mkoani Pemba, Wilaya ya Chakechake Pemba na Wilaya ya Wete Pemba na pamoja na visiwa vyote vya Pemba.

Mamlaka inaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya namna bora ya kutumia nishati ya umeme ikiwa ni pamoja na kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala, kutumia vifaa vinavyotumia umeme mdogo n.k. Aidha, Mamlaka inaendelea kusisitiza wananchi pindi wanapokuwa na malalamiko juu ya huduma za umeme kufika au kuwasiliana na Shirika la Umeme Zanzibar kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi na kutunza kumbukumbu zao vizuri. Ikitokea lalamiko lao halijafanyiwa kazi wasisite kuliwasilisha ofisi za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar iliyopo Maisara, Zanzibar.

mwisho.





" Ewe **mwananchi** epuka uvamizi wa Miundombinu ya umeme kwa kufanya shughuli ya kibiashara, kulima, kujenda makaazi kufanya hivyo ni hatari kwa maisha na mali zako.

**TUPIGIE**
**0772 877 879**



**ZECO** Tupo Kung'arisha Maisha Yako



# ZURA yashajihisha matumizi sahihi na salama ya Gesi ya kupikia (LPG) Zanzibar



**Na: Ahlam Saleh Khamis**

Matumizi ya kuni kwa ajili ya kupikia chakula ni jambo lililokuwa limezoeleka sana miongoni mwa jamii na ndio njia maarufu iliyokuwa ikitumiwa na wazee kabla na hata baada ya Mapinduzi ya Januari 1964.

Hata hivyo, tafiti mbalimbali zilizofanywa duniani, zimebainisha kuwa matumizi ya kuni yanaleta madhara makubwa kuliko faida kwa nchi husika na duniani kote. Kimsingi, ukataji ovyo wa misitu unaathiri kwa kiasi kikubwa mazingira na ni moja ya sababu zinazopelekea mabadiliko ya tabia ya nchi, hasa katika maeneo ambayo yapo karibu na bahari.

Takwimu zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 85 ya Watanzania hutumia bidhaa ya mkaa kwa ajili ya kupikia ambapo inakadiriwa kuwa zaidi ya tani milioni mbili za mkaa hutumika hapa nchini kwa ajili ya kupikia kwa mwaka na karibu nusu ya matumizi hayo yapo katika Jiji la Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFSA), Tanzania ina eneo la misitu lipatalo hekari 48.1 milioni lakini hekari 370,000 za misitu zinaharibiwa au kukatwa kila mwaka kwa ajili ya matumizi ya nishati ikiwemo ya kuni na mkaa.

Kwa upande wa visiwa vya Zanzibar inaelezwa kuwa hekari 1,000 za misitu zinaharibiwa kila mwaka kutokana na watu kukata miti ovyo kwa matumizi ya kuni na mkaa.

Hii inamaanisha kuwa eneo lote la misitu linaweza kuwa limemalizwa baada ya miaka 100 ijayo ikiwa kasi hii ya uharibifu na ukataji miti kwa ajili ya nishati itaendelea.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA) kwa kushirikiana na wadau wa Sekta za Usambazaji kubuni mbinu mbadala zitakazosaidia kupunguza na ikibidi kuondosha kabisa tatizo hilo.

Miongoni mwa jitihada za kuzuia hali hiyo kwa sasa ni pamoja na

Inaendelea Uk. 13




Wananchi wakipata elimu juu ya usalama sahihi wa matumizi sahihi na salama ya Gesi ya kupikia (LPG) katika kampeni ya jiko ni Gesi iliyoandaliwa na ZURA

kuhamasisha matumizi ya nishati ya gesi ya kupikia LPG ili kunusuru mazingira kuwa hatarini.

ZURA iliandaa Kampeni maalum ya mwaka wa 2022 kushajihisha matumizi ya Gesi ya kupikia kama moja ya jitihada hizo.

**KAMPENI YA 'JIKO NI GESI'**

(ZURA) iliandaa Kampeni maalum inayoitwa "JIKO NI GESI" kwa lengo la kutoa elimu na kushajihisha matumizi sahihi na salama ya gesi ya kupikia (LPG). Waandaaji wa Kampeni hiyo ni ZURA.Kampeni ya "JIKO NI GESI" ilijumuisha ushirikiano na ZEMA, Ministry of Health, Police Office, Plus Radio na Kampuni za gesi (ORYX, V-GAS, O-GAS, TAIFA GAS, na LAKE GAS) ilifanyika kuanzia Tarehe 19/03/2022 mpaka Tarehe 30/03/2022 katika Mikoa yote mitano (5) ya Zanzibar.

Dhamira ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) ni kusimamia huduma za Maji na Nishati (Umeme, Mafuta na Gesi ya kupikia - LPG) kwa uwazi na ufanisi kwa lengo kuchochea uwekezaji katika sekta za Maji na Nishati ili kuleta Maendeleo Zanzibar.

Umuhimu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) ya kufanya Kampeni hii ya "JIKO NI GESI" ni kuelimisha wananchi juu ya matumizi sahihi na salama ya nishati ya gesi ya kupikia (LPG) na kushajihisha utumiaji wa gesi badala ya kuni na mkaa ili kulinda afya za watumiaji, mazingira na kupunguza athari za tabia-nchi.

**SHUGHULI ZA KAMPENI YA "JIKO NI GESI" KAMPENI YA HEWANI (ON AIR)**

ZURA ilianza maandalizi ya kampeni kwa kurusha matangazo mawili (2) kwa siku kwa muda wote wa kampeni. Kufanya vipindi vinne (4) vya TV kupitia ZBC, ZCTV, ISLAND TV na ZINJIBAR ONLINE TV.

Inaendelea Uk. 14

Kufanya vipindi sita (6) vya redio kupitia ZBC REDIO, REDIO JAMII WILAYA YA KATI, REDIO JAMII TUMBATU, REDIO JAMII MTEGANI (MAKUNDUCHI), REDIO JAMII MKOANI na REDIO JAMII MICHEWENI.
Kwa upande wa mitandao ya kijamii ZURA iliweza kutuma taarifa (Post) pamoja na video fupi takriban thelathini (30) kwa siku kupitia FACEBOOK, INSTAGRAM, TWITTER, WHATSAPP na YOUTUBE CHANNEL ya ZURA.

**KAMPENI YA MITAANI (ROAD SHOW/ON GROUND)**
ZURA ikiambatana na wadau na kampuni tano (5) za gesi ilitembelea mikoa yote mitano (5) ya Unguja na Pemba kwa lengo la kukutana na wananchi kushajihisha matumizi na kutoa elimu kwa vitendo.

Maeneo yaliotembelewa kwa upande wa ***Mkoa wa Mjini Magharibi*** ni KWANYANYA, BUBUBU SKULI, GARAGARA, DARAJABOVU, SAATENI, AMANI, KIBANDA MAITI SOKONI, MIKUNGUNI, KISONGE, KIEMBE SAMAKI, MAUNGANI, MOMBASA SOKONI, M/KWEREKWE, KIJITO UPELE, KWARARA, FUONI na JUMBI.

Maeneo yaliotembelewa kwa upande wa ***Mkoa wa Kaskazi Unguja*** ni BUMBWINI, MFENESINI, KITOPE, MAHONDA, DONGE, MKOKOTONI, CHAAANI, KINYASINI, MKWAJUNI, KIVUNGE NUNGWI na KIWENGWA.

Maeneo yaliotembelewa kwa upande wa Mkoa wa Kusini Unguja ni MWERA, DUNGA, CHWAKA, UROA, JENDELE, PAJE, BWEJUU, JAMBIANI
Maeneo yaliotembelewa kwa upande wa Mkoa wa Kusini Pemba ni MACHOMANE, CHAKE SOKONI, CHANJAANI, CHANJAMJAWIRI, MTAMBILE, MTUHALIWA, MGAGADU, UWELENI, JONDENI na MKOANI SOKONI.

Inaendelea Uk. 15





Afisa huduma kwa wateja ZURA akitoa elimu kwa wananchi juu ya matumizi sahihi na salama juu ya Gesi ya kupikia

Maeneo yaliotembelewa kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini Pemba ni GOMBANI, MELI TANO, OLE KIANGA, MADENJANI, MWANE, MZAMBARAUNI, JUMBA KUBWA, UTAANI, BOPWE, KIZIMBANI na WETE SOKONI.

**MAMBO YALIOJITOKEZA**

ZURA iliweza kufanikisha malengo ya Kampeni hiyo kwa ushirikiano mkubwa kutoka kwa Wakuu wa Mikoa yote ya Zanzibar kwa kuhamasisha ushiriki wa Wananchi katika maeneo yao, Jeshi la Polisi kwa kutoa Ulinzi wakati wote wa Kampeni, Baraza la Sanaa kwa kutoa Kibali cha Gari la Matangazo, Jeshi la Zimamoto kwa kutoa Elimu ya kujilinda na kukabiliana na majanga ya moto na Mamlaka ya Mazingira kwa kutoa elimu ya mazingira na athari za kutumia kuni na mkaa.

Kwa upande wa Wananchi kulikua na muamko mkubwa sana ambapo Wananchi wengi walijitokeza katika Kampeni kwa kujifunza kwa vitendo utumiaji wa Gesi kwa usahihi na usalama pamoja na kujinunulia Majiko ya Gesi kutoka kwa Kampuni za Gesi.

Muda wa Kampeni ulikua mdogo kuweza kuyafikia maeneo mengi zaidi kwa Unguja na Pemba ambapo baadhi ya Wananchi walilazimika kusafiri kufuata elimu na huduma ya majiko ya gesi yaliyokua yanauzwa kwa bei ya punguzo ili kuongeza idadi ya Watumiaji wa Gesi Zanzibar.

**Maoni ya Wananchi kuhusu Matumizi ya Gesi**

Katika jitihada za kuimarisha utoaji huduma bora zaidi kwa wananchi, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar umefanya utafiti kwa wafanyabiashara na wateja wa huduma ya gesi ambao wameeleza yafuatayo: -

***Bwana Salum Sarahan mfanyabiashara wa bidhaa ya gesi maeneo ya Kisauni;***

Wananchi wengi wa Mjini wamekuwa na muamko

Inaendelea Uk. 16

wa kutumia nishati hiyo kutokana na kasi kubwa ya ongezeko la wanunuaji wa gesi kwenye duka lake; nishati ya gesi kwa kiasi kikubwa imesaidia kupunguza ukataji wa miti ovyo katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar.

Kwa kweli kama kanuni hizi zitaweza kufaya kazi na elimu ikishatuingia basi itasaidia sana kwani wapo wafanyabishara wengi wamekuwa hawazingatii usalama kwani wapo wanaochanganya biashara ya kawaida na gesi katika maduka yao bila kujali usalama wao na mali zao.

***Bibi Mwanakheir Salum mkaazi wa Maungani;*** Kupanda kwa bei ya gesi kunaweza kuleta athari kubwa kwa watumiaji na kunaweza pia kuleta athari za kimazingira na kiuchumi kwani asilimia kubwa ya wananchi hasa wanaoishi maeneo ya vijijini wanaweza kushindwa kununua bidhaa hiyo iwapo bei itaendelea kupanda.

Baadhi ya watu bado wanahofu ya matumizi ya nishati hiyo wakiamini kuwa inaweza kuripuka na kuwasababishia madhara, wakati nishati hiyo ni tofauti na ya zamani tayari imezimuliwa hivyo haiwezi kuripuka.

***Ali Masoud Meneja wa 'Khaify Trading CO - Taifa Gas Tanzania';*** Maeneo ya mjini yamaehamasika zaidi kwenye matumizi ya nishati ya gesi kutokana na uelewa wa matumizi pia kipato cha wanaoishi mjini kinaridhisha kutumia nishati hiyo. Tunaendelea kufanya jitihada za makusudi ili kufikisha gesi Mikoa yote pamoja na kuhakikisha kuwa inatumiwa kwa njia bora na sahihi.

ZURA iendelee kutoa elimu juu ya kanuni za gesi ili wafanyabiashara waweze kuzifahamu na pale wanapotaka kuuza nishati hiyo wawe wameshajiweka vizuri.

***Bahati Khalid Shaame;*** Natumia nishati ya gesi kwani inarahisisha matumizi pia ina tunza mazingira ya nyumba yangu. Nawaomba wanajamii wenzangu kutunza mazingira kwa kuepuka kukata miti kutokuwa na hofu juu ya matumizi ya nishati hiyo kwani nishati hiyo ni salama.

Mwisho.


## KAMPUNI YA MAENDELEO YA MAFUTA NA GESI ASILIA ZANZIBAR (ZPDC)

Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC) ni Kampuni yenye jukumu kuu la kushiriki katika shughuli za utafutaji na uchimbaji wwa Mafuta na Gesi Asilia kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.



**DKT. HUSSEIN ALI MWINYI**
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

**Kongamano la Kimataifa la Sekta ya Nishati na Viwanda Kufanyika kwa mara ya kwanza zanzibar**

ZPDC inatarajiwa kuwa mwenyeji wa Kongamano la Kimataifa la Sekta ya Nishati na Viwanda Zanzibar "Zanzibar Energy and Industry Summit (ZEIS)" linalolenga kuzitangaza fursa za uwekezaji Zanzibar kupitia Sekta ya Nishati, Viwanda pamoja na Uchumi wa Buluu.

Tarehe: 26 na 27 Julai, 2023
Mahali: Hoteli ya Golden Tulip Uwanja wa ndege Unguja.
Mgeni Rasmi: Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

Ili kushiriki katika kongamano hilo tafadhali tembelea tovuti ya
www.zan-eis.com

ZANZIBAR ENERGY & INDUSTRY SUMMIT

**"Mafuta na Gesi Asilia kwa Maslahi ya Wazanzibari"**





*Uwekezaji wa Nishati mbadala (Umeme wa jua) uliyopo Bwejuu Zanzibar*

# ZURA ni msimamizi na mtetezi wa wawekezaji wenye ufanisi

**Na: Mbarak Hassan Haji**

Majukumu kadhaa ya Mamlaka ya Kudhibiti huduma za Maji na Nishati (ZURA) yaliyotajwa kwenye Sheria Namba 7 ya mwaka 2013 iliyounda Mamlaka hiyo yamesisitiza kuwepo watoa huduma wenye kuzingatia vigezo na masharti ya usambazaji bidhaa na huduma zenye ubora wa viwango vinavyokubalika.

Majukumu haya yalianza kuwajengea hofu wafanyabiashara na hasa wawekezaji wakubwa ambao walikuwa wakifanya kazi kwa kujali zaidi maslahi yao kuliko kuzingatia ufanisi wa kutoa huduma na bidhaa zenye ubora.

Ili mambo hayo mawili – kutoa huduma na kujali ubora wa huduma – yapatikane, ni lazima kuwepo utaratibu madhubuti wa kusimamia matakwa na maslahi ya wateja, ambao wanahitaji wapatiwe bidhaa zenye ubora na kulinda uwezo wa wawekezaji wenye kuleta ufanisi katika shughuli zao. Kazi hii ya kuunganisha maslahi ya pande hizo mbili ndio iliyotekelezwa na ZURA kwa ujasiri mkubwa mara tu baada ya kuanzishwa kwa mamlaka hiyo.

Hata hivyo, kazi hii haikuwa rahisi kwani mara baada ya kuanzishwa kwa ZURA, kuliibuka hofu kubwa miongoni mwa wawekezaji kwa kudhani kuwepo kwa Mamlaka hiyo kutawanyima fursa ya kuendesha shughuli

Inaendelea Uk. 18



ZURA Zanzibar Utilities Regulatory Authority

zao kwa tija na kwamba Mamlaka itakuwa ikiwabana kiasi cha kuwanyima uwezo wa kupata faida katika biashara zao.

Miongoni mwa waliojenga hofu kubwa ni wawekezaji na wafanyabiashara wa bidhaa ya mafuta, ambao wengi wakidhani kwamba biashara ya mafuta Zanzibar itakufa kwa mwelekeo huo wa kudhibitiwa. Mawazo yaliyokuwepo ni kwamba bei ya mafuta itakuwa ikipangwa na ZURA kwa kumjali zaidi mtumiaji bila ya kuzingatia gharama za matumizi zinazotolewa na waendesha biashara hiyo.

Athari za hofu hiyo zilianza kujitokeza kwa kupelekea wafanyabiashara wengi wa mafuta Zanzibar kufikiria kusitisha kuagiza mafuta kwa kudhani kwamba kulikuwa hakuna haja ya kuendesha biashara hiyo kwa kuwa udhibiti mkubwa utakaofanyika utalenga zaidi kwa watumiaji kuliko kujali maslahi ya waagizaji.

Katika kukabiliana na suala hili, ZURA ililazimika kuwakabili wawekezaji kuwaeleza madhumuni ya kuundwa kwa taasisi hiyo pamoja na kuwatoa wasiwasi waliokuwa nao wafanyabiashara hao kwa kuwahakikishia kuwa biashara wanayoifanya ya bidhaa za mafuta ya petrol, dizeli na Mafuta ya taa itadhibitiwa kwa kuweka uwiano mzuri baina ya wawekezaji na watumiaji ambao ni wananchi.

Mkazo uliowekwa ni kuwakingia kifua wawekezaji kwa kuwahakikishia kwamba biashara watakayofanya itawaingizia faida, lakini katika kulindwa kwao huko kutatokana na kukubali kuwa watanufaika kwa Kulingana na hatua hiyo, ZURA wamefanikiwa kuweka utaratibu ambao unamuhakikishia mfanyabiashara anafaidika kwa huduma anayoitoa na mteja naye anapata bei inayostahiki kwa mujibu wa bei halisi za bidhaa hiyo katika soko la dunia.

Chini ya utaratibu huo, ZURA kwa ujasiri mkubwa ilifanikiwa kuondoa utata uliokuwepo, biashara ya mafuta imeimarika na inafanyika kwa uwazi kwa wafanyabiashara kuwa na uhakika na wanachokipata. Uwazi huo unakuwepo kwa

Inaendelea Uk. 19





kinachoingizwa, kinachosambazwa na kinachunguzwa ubora wake.

Utaratibu unaotumika kwa Zanzibar ni kuwa mafuta yanaagizwa na kuingizwa nchini kupitia kampuni nne zilizosajiliwa ambazo ni United Petroleumm (UP), GAPCO, Zanzibar Petroleum (ZP) na PUMA.

Kampuni hizo huwa hazinunui mafuta na kuyaleta Zanzibar moja kwa moja kutoka katika soko la dunia, bali huyanunua kupitia mfumo wa ununuaji wa pamoja wa mafuta Tanzania Bara (BPS) au kutoka Kenya kupitia mfumo uliowazi wa zabuni "Open Tender System" (OTS). Baada ya kuwasili katika Bandari ya Dar es Salaam, mafuta hayo husafirishwa na kuletwa Zanzibar, kutokana na unafuu wa uagiziaji wa mafuta kupitia mfumo huo wa uagiziaji wa pamoja.

Katika kumlinda mwekezaji na mtumiaji, Mamlaka inapanga bei kwa kuzingatia bei halisi na gharama zinazohusiana na uagiziaji, uhifadhi na usafirishaji wa mafuta hadi Zanzibar. Kuna vigezo tisa (9) vinavyotumiwa na ZURA katika kupanga bei ya mafuta, ambavyo ni:

i. Wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta duniani kwa mwezi husika wa uagizaji mafuta hayo.
ii. Gharama halisi za usafirishaji hadi katika Bandari ya Dar es Salaam, Bima na wastani wa faida ya muagiziaji wa mafuta, kwa mujibu wa Wakala wa Uagiziaji wa mafuta wa pamoja.
iii. Thamani halisi ya shilingi ya Tanzania kwa kulinganisha na dola ya Marekani.
iv. Tozo na ada mbali mbali zinazotozwa mafuta hayo katika Bandari ya Dar es Salaam kwa mafuta ambayo hayauzwi katika soko la ndani.
v. Gharama za kuhifadhi mafuta Tanzania Bara.
vi. Gharama za kuyaleta mafuta Zanzibar.
vii. Gharama za lazima zinazotozwa Bandarini Zanzibar.
viii. Kodi na ada zinazotozwa na Serikali kwenye biashara ya mafuta.
ix. Kiwango cha faida wanachokipata wauzaji wa jumla na reja reja.

Kwa mnasaba huo, ZURA imeweza kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Imekuwa ikiangalia na kudhibiti mwenendo mzima wa biashara ya mafuta Zanzibar. Taratibu za kisheria zinazingatiwa na zinafuatwa kikamilifu katika kuhakikisha kuwa mafuta yanakuwepo Zanzibar yakiwa na kiwango cha uhakika kwa ajili ya matumizi.

Hali hiyo ndiyo iliyopelekea, ndani ya kipindi kifupi cha miaka mitano (5), ZURA kuonekana imepiga hatua kubwa ya maendeleo katika biashara ya mafuta ikilinganishwa na ilivyokuwa huko nyuma.

**Umeme**

Kazi nyengine iliyofanywa na ZURA kwa ujasiri mkubwa ni ya kukitafutia

Inaendelea Uk. 20

ufumbuzi kilio cha muda mrefu cha upandaji holela wa bei ya nishati ya umeme pengine bila ya hata kuzingatia hali ya wateja. Tabia hiyo ilikuwa ikiwaathiri wananchi wengi ambao walikuwa wakiilalamikia sana kutokana na kufanyika karibu kila siku. Kilio hiki kimekuwepo muda mrefu, lakini hatimaye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweza kukipatia ufumbuzi kwa kuunda Mamlaka maalumu ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA). Moja ya jukumu kubwa la Mamlaka hii ni kuhakikisha inaangalia utolewaji wa huduma za uhakika na ambazo mwananchi wa kawaida anaweza kumudu kuzilipia.

Suala halikuwa ni utoaji wa huduma pekee, lakini jukumu jengine la ZURA, ni kuhakikisha Shirika ama taasisi inayozalisha ama kusambaza umeme nayo inaweza kupata faida kutokana na umeme unaouzwa kwa wananchi. Huo ni utaratibu wa kumkingia kifua mwekezaji lakini anatakiwa awe mwenye ufanisi. Kwa maana hiyo, ni lazima mtoa huduma na mnunuzi wa huduma ya nishati ya umeme walingane kimaslahi.

Hivyo, ZURA ililazimika kuangalia gharama za ununuaji wa nishati ya umeme kutoka kwa mzalishaji, usambazaji hadi kumfikia mtumiaji. Kuhusu kilio cha muda mrefu cha Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kuwapangia bei ya umeme wananchi, suala hilo hivi sasa limepatiwa ufumbuzi.

Chini ya utaratibu mpya uliowekwa, ZECO inapotaka kubadilisha bei ya umeme italazimika kupeleka maombi yao ZURA, ambayo itajadili maombi hayo kwa kuwashirikisha wadau wa Mamlaka na watakaotoa maoni ya kukubali au kupinga baada ya kusikiliza sababu za kusudio la kurekebisha bei kabla ya ZURA kuridhia ama kutoridhia kwa ombi hilo la kubadilisha bei ya umeme.

**Gesi**
Kwa kuwa gesi imeanza kuingia katika soko la Zanzibar ni dhamiri kuna wawekezaji wanaoendesha biashara hiyo na zipo kampuni mbali mbali hivi sasa zinauza bidhaa hiyo kwa wananchi.

Inaendelea Uk. 21



Katika kulifahamu hilo, serikali nayo imelazimika kuliwekea utaratibu maalumu. Kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), bidhaa ya gesi imewekewa utaratibu wa jinsi wawekezaji wakatavyoendesha biashara hiyo.

ZURA inaeleza kuwa, moja kati ya majukumu yake ni kuhakikisha kuwa bidhaa ya gesi kabla ya kumfikia mwananchi kwa ajili ya matumizi, inakuwa kwenye kiwango kizuri na salama. Aidha, jukumu jengine la ZURA katika kuisimamia nishati hiyo ni kuhakikisha kwamba wananchi wanaweza kuimudu bei inayouzwa bidhaa hiyo.

Sambamba na hilo, kampuni zenye kuuza gesi kwa ajili ya matumizi ya nishati ya kupikia nao wanafanya biashara hiyo kwa faida ikiwa ni jambo muhimu katika kulinda wawekezaji ili waweze kumudu kuifanya biashara hiyo kwa ufanisi.

ZURA imeshaanza kuwapatia leseni kampuni zenye kuingiza nishati ya gesi Zanzibar. Katika kuhakikisha kuwa ZURA inakuwa chombo imara zaidi, chenye kutegemewa kati ya wawekezaji na watumiaji (wananchi) hasa katika kufikia kiwango cha kimataifa kama zilivyo katika nchi nyengine nyingi duniani, ZURA imeandaa kanuni mbali mbali ambazo sasa zinatumika kwa ufanisi mkubwa na azma ya uimara wa chombo hicho utajitokeza kutokana na usimamizi na ufuatiliaji.

Ndani ya kanuni hizo mambo yatakayozingatiwa kwa uzito mkubwa ni viwango vya bidhaa na huduma zinazodhibitiwa, kuwepo vigezo na masharti ya usambazaji bidhaa na huduma na kuhakikisha kwamba watoa huduma wote wananufaika na kazi wanazozifanya na wana mtaji wa kutosha kwa kugharamia shughuli zao pia watumiaji hawaumii kwa bei wanayowekewa.

Mwisho.

## ZPRA
ZANZIBAR PETROLEUM (UPSTREAM) REGULATORY AUTHORITY

### HALI YA SASA YA SHUGHULI ZA MAFUTA NA GESI ASILIA- ZANZIBAR

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliingia katika makubaliano ya kwanza ya kugawana uzalishaji (PSA) pamoja na kampuni ya RAKGAS ya Ras al Khaimah tarehe 23 Oktoba mwaka 2018 kwa Kitalu cha Pemba, Zanzibar kwa jumla ya eneo za kilomita za mraba 11,864 kwa kazi ya utafutaji na uchimbaji Mafuta na Gesi Asilia. Shughuli hizo za kitafiti kupitia PSA hiyo zilijumuisha kazi zifuatazo:-

Uchunguzi wa mvuto wa Tensa (FTG) ulifanyika takribani kwa wiki sita (6), Utafiti wa 2D Seismic ulifanywa Pemba na Zanzibar ulianza Novemba, 2017, na kumalizika Februari 2019. Kampuni ya BGP ilipewa mkataba mdogo na RAKGAS ilikufanikisha uchunguzi huo . Uchunguzi wa 2D Seismic ulifanyika baharini, ufukweni na katika sehemu za mipaka ya Pemba na Zanzibar. Takribani kilomita za mistari 3776.6 ilichukuliwa katika uchunguzi. Kilomita za mistari kwa kila eneo kama ifuatavyo:-

Baharini- Kilomita 2815
Ufukweni –Kilomita 712
Sehemu za mipakani –Kilomita 158

Matokeo ya awali yalionyesha uwepo wa Gesi Asilia takribani futi za ujazo wa cubic trillion 3.8 ndani ya Pemba- Zanzibar.

zpra Zanzibar zpraznz zpraznz

## ZPRA
ZANZIBAR PETROLEUM (UPSTREAM) REGULATORY AUTHORITY

### UTANGAZAJI WA VITALU VIPYA VYA MAFUTA NA GESI ASILIA

Kufuatia kukabidhiwa data za Mafuta na Gesi Asilia kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA), ilisaini mkataba na Kampuni ya Kimataifa ya Schlumberger mnamo tarehe 4 Novemba, 2022 kwa lengo la kuzitafsiri data hizo ili kuweza kufanikisha kazi ya ugawaji wa utangazaji wa Vitalu vipya vya uwekezaji katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

Utekelezaji wa Mkataba huo umeenda vizuri ambapo kazi ya kutafsiri data na kugawa Vitalu vipya vya uwekezaji katika eneo la Bahari kuu imekamilika. Kukamilika kwa kazi hiyo kunaipa nafasi nzuri Wizara kutangaza maeneo mapya ya uwekezaji katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar ndani mwaka 2023.




PBZ IKHLAS
Isikupite Fursa Hii
PBZ IKHLAS inakuwezesha kumiliki USAFIRI wa ndoto yako kwa gharama nafuu
IKHLAS
kwa Faida Halali
pbzbank
pbzbank_
PBZBANK



# ZURA yatandika uwanja wa ushindani wa kukuza uchumi

*Mradi wa Maji safi na salama uliyopo Kidutani Zanzibar*

**Na: Mbarak Hassan Haji**

Dhamira kuu ya kuanzishwa Mamlaka ya Uthibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA) ni kuwa na chombo kinachosimamia huduma za nishati na maji kwa uwazi na ufanisi ili kukuza uwekezaji utakaochangia maendeleo ya kiuchumi Zanzibar.

Kuwepo kwa dhamira hiyo, kunakusudia kutandika uwanja kwa wawezekaji na wafanyabiashara wa sekta hizo za maji na nishati kushindana kulikamata soko kupitia njia za halali, wateja wakiwa ni wafalme katika ushandani huo.

Lengo hasa ni kutimiza azma ya kudhibiti sekta za maji na nishati kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa huduma hizo zinatolewa ipasavyo kwa watumiaji kupata huduma zinazostahiki na wafanyabiashara kunufaika kihalali kutokana na biashara zao ili kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Kazi inayofanywa na ZURA ni kutayarisha taratibu za kuwepo ushindani mzuri na kushajiisha sekta binafsi kushiriki katika uwekezaji kwenye taasisi zinazotoa huduma kwa kuhakikisha taasisi zinatekeleza shughuli zao kwa mujibu wa Sheria. Mamlaka ililazimika kuandaa na kutekeleza utaratibu unaohakikisha kwamba wenye leseni wanatoa huduma kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa na kanuni na sheria na kwamba hakuna mbinu, hila na udanganyifu wowote unaofanywa na wenye leseni katika kulipa kodi au kufanya shughuli

Inaendelea Uk. 24





ZURA

Uwekezaji Mpya wa kampuni ya United Petroleum (UP) uliyopo Mangapwani Unguja

alizokuwa hajaruhusiwa. Aidha, katika kudhibiti huduma hizo kwa ukamilifu, Mamlaka imesisitiza kufuatwa misingi ya maadili, ukweli wa utoaji taarifa, muundo wa utumishi pamoja na haki na wajibu wa wafanyakazi walioko katika sekta hizo.

Ili sheria zitawale ushindani huo, ZURA inajitahidi kuziba mianya iliyokuwa ikiruhusu kufanyika biashara haramu na kuweka miongozo ya kusimamia uendeshaji wa utoaji wa huduma zote kwa uwazi, ufanisi na kwa usawa kwa kila mwekezaji na mfanyabiashara.

Juhudi zote hizi zilizofanywa na ZURA zilikusudia kuwepo utaratibu unaofahamika wa kuendesha shughuli za sekta ya maji na nishati ili kuifanya sekta hiyo kuimarika zaidi katika kukuza uchumi na kuendeleza ustawi wa jamii nchini.

Kwa muda mrefu, uchumi wa Zanzibar ulikuwa unategemea sana sekta ya uwekezaji na hasa uuzaji wa bidhaa zinazotokama na nishati. Biashara ya mafuta na petroli, dizeli na mafuta ya taa imekuwa ikichangia sana uchumi utokanao na mauzo ya ndani.

Hali ya mwenendo wa uchumi nchini unaonesha kwamba uchumi wa Zanzibar unaelekea katika utoaji huduma zaidi kuliko uzalishaji. Hii imedhihirika katika mwenendo wa mchango wa sekta za huduma katika Pato la Taifa, ambapo mchango wa sekta za huduma zikiwemo za biashara na utalii kufikia wastani wa

Inaendelea Uk. 25



zaidi ya asilimia 45. Kukua kwa mchango wa sekta za huduma kunatokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali na sekta binafsi katika sekta hizi na hasa miundombinu inayosaidia kukuza sekta mbalimbali nchini, biashara ya mafuta ikiwa na mchango mkubwa wa mafanikio hayo. Uwekezaji mkubwa katika utoaji huduma za usafiri na mahoteli ni miongoni mwa maeneo ambayo yameinyanyua sekta ya huduma na kuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa.

Kuundwa kwa Mamlaka hii, kumetokana na matakwa ya Sera ya Maji ya Mwaka 2004, ambayo imetaka Wananchi kuchangia Huduma ya Maji na sera ya Nishati ya Zanzibar ya mwaka 2009, ambayo imeeleza haja ya kuwepo mdhibiti anayejitegemea wa Sekta ya Nishati. Mageuzi hayo ya Sekta za Maji na Nishati yamo katika Mpango Mkuu wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA) pamoja na Dira ya Maendeleo ya miaka ya thalathini (vision 2050). Moja kati ya kazi zinazotekelezwa na ZURA kwa mafanikio ni kuendeleza mageuzi ya kiuchumi, kifedha na kiutawala kwa madhumuni ya kukuza uchumi utakaokuwa endelevu kulingana na Dira 2050. Dira hii ndio iliyotoa mwangaza wapi Zanzibar ielekee katika kukuza uchumi wake na



Bodi ya Wakurugenzi wa ZURA ukifanya ziara katika kisiwa cha Njau Pemba kujionea hali halisi ya Mradi wa Umeme wa jua unaotoa huduma katika kisiwa hicho

kushughulikia maslahi ya wananchi kiustawi wa jamii.

Tokea kuanzishwa, ZURA imekuwa ikifanya kazi kulingana na mageuzi hayo ya kiuchumi, kifedha na kiutawala kwa madhumuni ya kukuza uchumi utakaokuwa endelevu kwa kushajiisha wawekezaji kuzingatia udhibiti bora wa fedha za Serikali.

Kati ya malengo ambayo ZURA imejiwekea kuyatekeleza ni pamoja na kuhamasisha wawekezaji, wafanyabiashara na wananchi katika kuelewa umuhimu wa kukusanya fedha na uwajibikaji wa kila mhusika juu ya suala la mapato.

Inaendelea Uk. 26



Pamoja na kazi hiyo, ZURA imefanikiwa kushajiisha wawekezaji kuweka vitega uchumi vyao nchini kwa lengo la kuipatia nchi mapato zaidi, kupunguza tatizo la ajira kwa vijana na kuingiza nchini teknolojia ya kisasa.

Maendeleo hayo yamesaidia kuiweka nchi katika mazingira bora zaidi ya kiuchumi, utawala bora, na kiuwekezaji unaozingatia ufanisi katika uimarishaji utawala bora. Mafanikio hayo hatimaye yalielekezwa kwenye masuala ya kifedha, kiutawala na uchumi wenye nguvu.
Ni dhahiri kwamba ndani ya kipindi hiki tokea ZURA kuasisiwa, kumekuwa na matokeo mengi ambayo yalisababisha mabadiliko ya kiuchumi kwa jumla, mabadiliko ya maisha ya wananchi, pamoja na mabadiliko katika upatikanaji wa huduma bora kwa jamii.

Kuongezeka kwa thamani ya utoaji huduma nchini kumechangia kukuza Pato la Taifa ambalo nalo huchangia kukua kwa kiwango cha wastani wa pato kwa kila mtu.

Kwa kuangalia kazi zilizofanywa, hapana shaka ZURA imechangia katika kuleta maendeleo ya kiuchumi kwa kudhibiti kikamilifu sekta ya Maji na Nishati kijamii ili kuhakikisha Serikali kupitia Mamlaka hii, huduma zake zinawafikia wananchi moja kwa moja.

Hivyo, Mamlaka hii inaonekana wazi wazi jinsi inavyohusika moja kwa moja katika kuleta maendeleo ya kiuchumi, kutokana na kusimamia na kuratibu shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii ikiwemo kudhibiti, kutoa leseni, kupanga bei, ukusanyaji wa mapato pamoja na huduma nyingine za kiuchumi na kijamii.

Mwisho.



Mkaguzi wa Mafuta kutoka ZURA akikagua ubora wa Mafuta katika kituo cha Jambiani Unguja

WIZARA YA AMJI NISHATI NA MADINI

# TARATIBU ZA UOMBAJI WA KIBALI CHA MCHANGA

## HATUA YA KWANZA: JISAJILI

1. Tembelea tovuti ya https://madinismz.go.tz
2. Tafuta kitufe kilichoandikwa "SAJILI"
3. Chagua aina ya maombi unayotaka
   - Mtu binafsi ataruhusiwa kuomba si zaidi ya tani 30
   - Kampuni au viwanda ataruhusiwa kuomba si zaidi ya tani 50
   - Mahitaji ya miradi ataruhusiwa kuomba si zaidi ya tani 2,000
4. Ingiza nambari za kitambulisho cha Mzanzibar kwa matumizi binafsi, kwa matumizi ya kiwanda na miradi, muombaji ataingiza namba ya cheti cha usajili wa kampuni (BPRA), Tin Namba pamoja na cheti cha mlipa kodi cha ZRB (VRN Number)
5. Bonyeza "Thibitisha Kitambulisho"
6. Hakiki taariza zako, rekebisha inapobidi. Ukimaliza bonyeza "Sajili"

## HATUA YA PILI: MAOMBI YA KIBALI

1. Tembelea tovuti ya https://madinismz.go.tz
2. Weka nambari ya simu pamoja na PIN kama ulivyopokea kupitia ujumbe mfupi kwenye simu yako.
3. Bonyeza "Ingia"
4. Baada ya kufunga, tafuta kitufe kilichoandikwa "Omba Kibali"
5. Jaza taarifa zote zinazohitajika ikiwemo eneo, eneo la ujenzi, sababu ya kibali, kiwango (tani) unachohitaji n.k
6. Bonyeza "Endelea".
7. Chagua gari utakazotumia.
8. Bonyeza "Wasilisha"
9. Bonyeza kitufye kilichoandikwa "Maombi".
10. Bonyeza "Angalia".
11. Bonyeza "Ankara"
12. Lipa gharama ya maombi kwa njia ya EzyPesa, TigoPesa au PBZ Bank.
13. Ofisi itafanya taratibu zake za kiofisi (approval)
14. Utatumiwa ujumbe katika simu yako ya kulipia tani za mchanga ulizokubaliwa.
15. Utarudi katika akaunti yako ya mfumo na kuona hali ya maombi imebadilika na kuruhusiwa kulipa tani zako ulizoruhusiwa au kukubaliwa na ofisi
16. Utalipa tani ulizoruhusiwa na utapokea ujumbe wa malipo uliyoyafanya
17. Utapata kibali chako kwa ajili ya matumizi.

WWW.madinismz.go.tz

wmnm_znz

wmnmznz




# ZURA YATUMIA MFUMO WA UDHIBITI (ZIRS)

**Na: Ahlam Saleh Khamis**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar, sasa yafanyakazi zake za udhibiti kwa kutumia mfumo.

Mamlaka imelazimika kubadilisha kazi zake kutoka kimawakaratasi na kwenda online. Mfumo huo wa ZURA Integrated System- ZIRS, unawarahisishia wateja kuweza kufanya maombi ya leseni, kufanyika kwa ukanguzi wa miondombinu ya na nishati kwenye mfumo, kuwapatia watoa huduma ripoti ukanguzi kupitia mfumo na mrejesho juu ya kanguzi hizo. Mfumo huu unajumuisha mambo yafuatayo:
'Online Licence and Tariff Application System -OLTAS'
Sehemu hii ya mfumo huwarahisishia watumiaji kuweza kufanya maombi ya leseni na kuomba mabadilisho ya bei za huduma tunazozidhibiti. Ili kuweza kupatiwa leseni hizo n abei kwa ajili ya utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Aidha kwa mfumo huu kutawezesha kufanyika kazi kwa haraka na ufanisi zaidi kwa watoa huduma wa maji na nishati.

'Regulator Performance Management System- RPMS'
Sehemu hii ya mfumo ni kwajili ya ukanguzi wa miundombinu ya maji na umeme kwa kuhakikisha usalama na ubora wa huduma hizo kwa wananchi. Mfumo unatoa ripoti za ukanguzi na kuwapatia watoa huduma mrejesho wa marekebisho ambayo yameonekana ndani ya kanguzi hizo.
'National Petroleum and Gas Information System- NPGIS'




Sehemu hii ya mfumo ni kwajili ya ukanguzi wa miundombinu ya mafuta na gesi kwa kuhakikisha usalama na ubora wa huduma hizo kwa wananchi. Mfumo unatoa ripoti za ukanguzi na kuwapatia watoa huduma mrejesho wa marekebisho ambayo yameonekana ndani ya kanguzi hizo.

'Integrate Regulator Dashboard – IRD'

Sehemu hii ya mfumo inamjumuisho wa sehmu sote tatu OLTAS, RPMS na NPGIS na kupata taarifa za ripoti zote za ukanguzi, ripoti za utoaji wa leseni, ripoti za uingzaji wa mafuta na idadi ya mafuta yaliyopo nchini.



# UFAHAMU MFUMO WA KUTOLEA RISITI ZA KIELEKTRONIKI (VFMS)

## VFMS ni nini?

Virtual Fiscal Management System (**VFMS**) ni mfumo wa kisasa wa utoaji wa Risiti za Kielektroniki unaotumia Teknolojia ya kisasa ambayo ni rahisi kwa wafanyabiashara wa aina mbali mbali na kutegemewa kuongeza kiwango cha mapato ya Serikali sambamba na kupunguza udanganyifu katika utoaji wa Risiti.

## Ni lipi lengo la mfumo wa VFMS?

Mfumo wa VFMS umeanzishwa kwa lengo la kuhifadhi taarifa za mauzo, kutoa ripoti za mauzo na kuwawezesha wafanyabiashara kutoa Risiti ili kuongeza urahisi na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

## Ni zipi Faida za mfumo wa VFMS?

Miongoni mwa faida za mfumo huu ni:

- ☑ Kuongeza pato la Serikali.
- ☑ Kuondosha Risiti za kuandikwa kwa Mkono.
- ☑ Kuwa na taarifa za mwenendo wa biashara na wafanyabiashara.
- ☑ Kumpa wepesi mfanyabiashara katika uhifadhi wa kumbukumbu zake.
- ☑ Kuona miamala ya mauzo kwa wakati halisi.

**Dai Risiti ya Kielektroniki Kila Ukifanya Manunuzi**

**Tulipe Kodi Kwa Maendeleo Ya Zanzibar**

# JEE! WAJUA



Mamlaka ina utaratibu wa kupokea na kuyashughulikia malalamiko kwa upana zaidi na umahiri wa hali ya juu.

## Nani anaweza kuwasilisha lalamiko?

a) Muhusika (mtu mwenyewe mwenye lalamiko).
b) Mtu aliyechaguliwa kufungua malalamiko kwa niaba ya watu wengine.
c) Sheha wa shehia husika ikiwa ni lalamiko la mtu zaidi ya mmoja ndani ya shehia hiyo.

## Zijue njia za kuwasilisha lalamiko.

i. Kuwasilisha lalamiko katika ofisi za ZURA.
ii. Kujaza fomu ya malalamiko inayopatikana katika tovuti ya ZURA.
iii. Kupiga simu au kutuma SMS kwa namba **+255 774 871 212.**



**MAJI**

Mlalamikaji anatakiwa awasilishe lalamiko lake Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kwa maandishi au kwa kupiga namba ya huduma kwa wateja **+255 774 778 888**, iwapo hakuridhika, amechelewa kupatiwa ufumbuzi au amekosa kupatiwa ufumbuzi wa lalamiko lake, anatakiwa awasilishe lalamiko hilo **ZURA**.



**UMEME**

Mlalamikaji anatakiwa awasilishe lalamiko lake Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kwa maandishi au kwa kupiga namba ya huduma kwa wateja **+255 772 877 879,** iwapo hakuridhika, amechelewa kupatiwa ufumbuzi au amekosa kupatiwa ufumbuzi wa lalamiko lake, anatakiwa awasilishe lalamiko hilo **ZURA**.



**MAFUTA**

Mlalamikaji anatakiwa awasilishe lalamiko lake kwa mtoa huduma wa Mafuta na kutoa taarifa **ZURA** ndani ya masaa 48 baada ya kuwasilisha lalamiko lake, ili ukaguzi wa kitaalamu uweze kufanyika kwa haraka katika eneo husika (Kituo cha Mafuta). Mlalamikaji analazimika kuwa na Stakabadhi (Risiti) ambayo ndio itakua kielelezo (ushahidi) wa lalamiko lake.



**GESI YA KUPIKIA (LPG)**

Mlalamikaji anatakiwa awasilishe lalamiko lake kwa mtoa huduma wa Mafuta na kutoa taarifa **ZURA** ndani ya masaa 48 baada ya kuwasilisha lalamiko lake, ili ukaguzi wa kitaalamu uweze kufanyika kwa haraka katika eneo husika (Kituo cha Mafuta). Mlalamikaji analazimika kuwa na Stakabadhi (Risiti) ambayo ndio itakua kielelezo (ushahidi) wa lalamiko lake.